

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**



S.L.P 42325,  
Simu Nambari: 2850633  
Nukushi: (022) 2850635  
Barua Pepe: [rbctemeke@pccb.go.tz](mailto:rbctemeke@pccb.go.tz)  
Wavuti: [www.pccb.go.tz](http://www.pccb.go.tz)

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**TEMEKE JUNI 3, 2020**

**TAKUKURU TEMEKE YAIKABIDHI AFYA TEMEKE SACCOS KIASI CHA  
SHILINGI 241,303,313/=**

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoa wa Temeke, Jijini Dar Es Salaam ilipokea fedha Shilingi 241,303,313/= kutoka kwa Dunstan Sebastian Kabelwa aliyekuwa Meneja wa Afya – Temeke Saccos na Vailet Francis Chengula aliyekuwa Karani wa fedha wa Afya Saccos. Fedha hizo ziliokolewa kufuatia uchunguzi uliofanywa na TAKUKURU (M) Temeke jijini Dar Es Salaam na kubaini upotevu mkubwa wa fedha katika Saccos hiyo.

Awali mnamo tarehe 7/6/2018 Ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Temeke ilipokea malalamiko yanayohusu ubadhirifu wa fedha za michango ya wanachama wa Afya Temeke Saccos iliyopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke uliofanywa na watendaji wa Saccos hiyo.

Uchunguzi wa tuhuma hii ulianza na kubaini ubadhirifu wa fedha za Saccos uliofanywa na watuhumiwa. Baada ya watuhumiwa kuhojiwa kulingana na ushahidi uliokusanywa, walikubali kurudisha fedha hizo.

Leo tarehe 03/06/2020 TAKUKURU (M) Temeke inayo furaha kukabidhi fedha hizo kiasi cha shilingi **241,303,313/=** kwa uongozi mpya wa Afya Saccos. Kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi **35,285,500/=** kitakabidhiwa kwa baadhi ya wanachama wa Saccos hiyo. Wanachama watakaokabidhiwa hapa leo ni baadhi ya wastaafu **10** waliokuwa wanachama wa Saccos hiyo.

Aidha fedha zilizobakia zitaingizwa katika akaunti ya chama hicho kwa ajili ya kuendelea na malipo kwa wanachama wengine waliokuwa wanadai.

TAKUKURU Mkoa wa Temeke inatoa wito kwa wananchi wote kuendelea kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kupitia mitandao yote ya simu kwa kupiga au kutuma ujumbe mfupi kwa namba ya bure 113 au kupiga 113 au kufuata maelekezo au fika katika ofisi ya TAKUKURU iliyopo karibu nawe.

**JENGA NCHI YAKO KATAA RUSHWA**

Imetolewa na:

**Donasian Kessy**

**Mkuu wa TAKUKURU (M)**

**Temeke**